**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TANGAZO LA MWALIKO KWA WAANGALIZI WA NDANI WA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA CHAMWINO, HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO NA MADIWANI KATIKA KATA 11 ZA TANZANIA BARA

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Chamwino lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma na Madiwani katika kata 11 za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumatano tarehe 04 Novemba, 2026 katika Jimbo na kata zifuatazo: -

**A: Jimbo Litakalofanya Uchaguzi mdogo wa Ubunge**

| Mkoa | Halmashauri | Jimbo |
|---|---|---|
| Dodoma | Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino | Chamwino |

**B: Orodha ya Kata Zitakazofanya Uchaguzi Mdogo wa Madiwani**

| Na. | Halmashauri | Kata |
|---|---|---|
| 1. | Halmashauri ya Jiji la Mbeya | Nonde |
| 2. | Halmashauri ya Mji Njombe | Lugenge |
| 3. | Halmashauri ya Mji Mbulu | Bargish |
| 4. | Halmashauri ya Wilaya ya Muheza | Makole |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Pangani | Mwera |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro | Oldonyosambu |
| 7. | Halmashauri ya Wilaya ya Uyui | Igalula |
| 8. | Halmashauri ya Wilaya ya Iramba | Shelui |
| 9. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa | Mvumi |
| 10. | Halmashauri ya Wilaya ya Tarime | Nyarero |
| 11. | Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe | Ilolangulu |

Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 13(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa waangalizi wa ndani wa uchaguzi wenye nia ya kuangalia uchaguzi.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi za ndani zenye nia ya kuangalia uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Chamwino, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na Madiwani katika kata 11 za Tanzania Bara kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi zenye nia ya kuangalia uchaguzi huo ziwasilishe maombi kwa kutumia kiunganishi (*link)* kifuatacho: https://ams.inec.go.tz

Barua ya maombi itapaswa kuainisha mambo yafuatayo: -

i. anuani kamili ya taasisi au asasi husika;

ii. mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi (*Physical address*);

iii. shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;

iv. sehemu ambazo taasisi au asasi inapenda kwenda kuangalia uchaguzi;

v. idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi;

vi. majina na namba za simu za viongozi watatu wa taasisi au asasi husika;

vii. ikiwa taasisi au asasi ya ndani inahusisha viongozi ambao si raia wa Tanzania, viongozi wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa ni lazima wawe watanzania;

viii. nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na

ix. nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 26 Septemba, 2026 hadi tarehe 02 Oktoba, 2026.

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 02 Oktoba, 2026.**

**Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la uangalizi wa uchaguzi kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.**

**Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa katika tangazo hili hayatafanyiwa kazi.**

Limetolewa leo tarehe 25 Septemba, 2026 na:

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**